TANGAZO LA SERIKALI NA. 945 la tarehe 29/11/2019

SHERIA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA,
(NA. 5 YA MWAKA 2019)

AGIZO

(Imetolewa kwa mujibu wa kifungu Na.29(1) (d))

AGIZO LA MAREKEBISHO YA BEI YA MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA MUGUMU (MUGUMU WSSA), 2019

Kichwa cha Agizo

1. Agizo hili litajulikana kama, Agizo la Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mugumu("MUGUMU WSSA"), (la Kurekebisha Bei za Huduma za Maji safi na Usafi wa Mazingira), la Mwaka 2019.

Tarehe ya Kuanza kutumika

2, Agizo hili litaanza kutekelezwa rasmi kuanzia tarehe 1 Disemba 2019.

Marekebisho ya Bei

3. Bei za majisafi na usafi wa mazingira za Mugumu WSSA zinarekebishwa kulingana na Jedwali la Kwanza katika Agizo hili.

Masharti

4. Bei zilizoidhinishwa zitaambatana na masharti yafuatayo:

(a) kabla ya kuanza kutekeleza bei mpya, Mugumu WSSA iwasilishe EWURA vielelezo kwamba ilitoa taarifa kwa wateja wake kuhusu bei mpya za huduma zake na pia ilitoa elimu kikamilifu kwa umma ikiwa ni pamoja na wawakilishi wa wananchi, serikali na viongozi wa dini katika eneo lake la huduma;

(b) Mugumu WSSA ihakikishe inanunua na kuweka stoo dira za kutosha kwa ajili ya kubadilisha zilikwisha muda wake ili zoezi la ubadilishwaji wa dira lifanyike kwa kipindi kifupi;

(c) Ifikapo tarehe 31 Januari 2020 au kabla, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mugumu itawasilisha EWURA Mpango wake wa Kibiashara

uliopitiwa upya kwa kuzingatia bei zilizoidhinishwa na mpango wa utekelezaji wa masharti ya Agizo hili;

(d) Mamaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mugumu ihakikishe kuwa inazingatia matakwa ya kukusanya tozo ya udhibiti na kuiwasilisha EWURA;

(e) Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mugumu itawaunganisha wateja wake wote dira za maji ifikapo 31 Desemba 2019. Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mugumu inatakiwa kununua dira za maji za kutosha ili kutekeleza agizo hili;

(f) ifikapo tarehe 30Novemba 2019 au kabla, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mugumu iwasilishe EWURA mkakati wa kupunguza upotevu wa maji kutoka 33% za sasa hadi 22% ifikapo 2021/22;

(g) ifikapo tarehe 31 Desemba 2019 au Kabla, Mugumu WSSA iandae mpango wa kuwabaini wateja wasiojiweza waliopo katika eneo lake la huduma na kuwapatia huduma ya maji kwa namna iliyo nafuu;

(h) ifikapo tarehe 31 Desemba 2019 au kabla Mugumu WSSA iandae na kuwasilisha EWURA mpango wa kuwafikia wateja wake kwa lengo la kutoa elimu juu ya Huduma za maji;

(i) Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mugumu, kwa kutumia mapato yatokanayo na bei zilizoidhinishwa, itatekeleza miradi iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Agizo hili;

(j) Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mugumu itafikia viashiria vya utendaji kama ilivyooneshwa kwenye Jedwali la Tatu la Agizo hili;

(k) Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mugumu, kwa kila mwaka kama sehemu ya taarifa yake ya utendaji ya mwaka, itawasilisha taarifa ya utekelezaji wa masharti yaliyopo kwenye Agizo la Bei na kila kifungu cha gharama katika mahitaji ya fedha yaliyoidhinishwa kama yalivyoainishwa katika Jedwali la Nne; and

(l) Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mugumu itaendelea kuwasilisha EWURA taarifa

zake za fedha na utendaji kwa mujibu wa matakwa ya EWURA. Taarifa hizi zitatumiwa na EWURA katika kufanya tathmini ya utendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mugumu ikilinganishwa na Mamlaka nyingine za Majisafi na Usafi wa Mazingira na uboreshaji wa huduma zake. Pia EWURA itazingatia tathmini hii katika kufanya maamuzi ya maombi yote yatakayowasilishwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mugumukatika siku zijazo.

Utenguzi wa Agizo Na. 11-014 la mwaka 2011

5. Agizo hili linatengua matumizi ya Agizo Na. 11-014 la mwaka 2011.

_____

MAJEDWALI

_____

JEDWALI LA KWANZA

(Limetengenezwa chini ya aya ya 3)

BEI NA ADA ZILIZOIDHINISHWA

Jedwali Namba 1(a): Bei za Maji za Sasa na Zilizoidhinishwa kwa Wateja Wenye Dira (Shilingi/ Mita ya Ujazo)

Aina ya Mteja	Bei za Sasa	Bei zilizoidhinishwa		
	2018/19	2019/20	2020/21	2021/22
Majumbani	540	810	1,053	1,158
Biashara	550	825	1,073	1,180
Taasisi	560	840	1,092	1,201
Viwanda	-	900	1.170	1,287
Magati	500	750	975	1,073
Wastani wa bei		825	1,073	1,180

Jedwali Namba 1(b): Bei za Maji za Sasa na Zilizoidhinishwa kwa Wateja Wasio na Dira (Shilingi/ Mwezi)

Kundi la Wateja	Bei za Sasa	Bei zilizoidhinishwa		
	2018/19	2019/20	2020/21	2021/22
Majumbani	7,500	Haijaidhinishwa		
Taasisi	11,000			
Biashara	16,000			
Viwanda	-			
Magati	16,000			

Jedwali Namba 1(c): Ada ya Sasa na Iliyoidhinishwa ya Maunganisho ya Maji Safi (Shilingi/Maunganisho)

Kundi la Wateja	Ada ya sasa	Ada zilizoidhinishwa		
	2018/19	2019/20	2020/21	2021/22
Majumbani	Asilimia 20 ya gharama za vifaa na ufundi	Asilimia 20 ya gharama za vifaa na ufundi kama ilivyobainishwa katika Kanuni za Majisafi za mwaka 2013		
Taasisi				
Biashara				
Viwanda				
Magati				

Jedwali Namba 1(d): Ada ya Sasa na Iliyoidhinishwa ya Kurejeshewa Huduma ya Maji Baada ya Kukatiwa (Shilingi/Kurejeshewa Huduma)

Aina ya Mteja	Ada za sasa	Ada Zilizoidhinishwa		
	2018/19	2019/20	2020/21	2021/22
Majumbani	10,000	15,000	15,000	15,000
Taasisi	10,000	15,000	15,000	15,000
Biashara	10,000	15,000	15,000	15,000
Viwanda	-	15,000	15,000	15,000
Magati	10,000	15,000	15,000	15,000

JEDWALI LA PILI

(Limetengenezwa chini ya aya ya 4(i))

MIRADI ITAKAYOTEKELEZWA

Kazi Zitakazotekeezwa	Shilingi za Kitanzania (Milioni)			Maoni
	2019/20	2020/21	2021/22	
Matengenezo				
Kubadilisha Dira za maji 1,000 katika mwaka 2019/20, 812 katika 2020/21 na 625 katika mwaka 2021/22	80.0	65.0	50.0	Utekelezaji utafanyika kabla ya tarehe 30 Juni, 2022
Kubadilisha "gate valves "6 2019/20 (10); mwaka 2020/21 (10), na 2021/22, (8).	30.0	30.0	24.0	Utekelezaji utafanyika kabla ya tarehe 30 Juni, 2022
Kubadilisha *polypipes rolls* "2" in 2019/20, 5; 2020/21, 5; 2021/22, 5	3.75	3.75	3.75	Utekelezaji utafanyika kabla ya tarehe 30 Juni, 2022
Jumla Ndogo (Matengenezo)	113.75	98.75	77.75	
Uwekezaji Mpya				
Kununua Dira ndogo mpya za maji 200 katika mwaka 2019/20, Dira 300 katika 2020/21, na Dira 400 katika 2021/22	12.0	18.0	24.0	Utekelezaji utafanyika kabla ya tarehe 30 Juni, 2022
Kujenga matangi mawili yenye ukubwa wa mita za ujazo 200 katika maeneo ya Kisangura na Burunga	0	180.0	220.0	Utekelezaji utafanyika kabla ya tarehe 30 Juni, 2022
Kuunganishia wateja wapya 150 kila mwaka kwa gharama ya TZS 60,000 kwa kila mteja	9.0	9.0	9.0	Utekelezaji utafanyika kabla ya tarehe 30 Juni, 2022
Jumla Ndogo – Uwekezaji Mpya	21.0	207.00	253.00	
JumlayaUwekezajiWote	134.75	305.75	330.75	

JEDWALI LA TATU

(Limetengenezwa chini ya aya ya 4(j))

VIASHIRIA VYA UTENDAJI

Maelezo	Uniti	Lengo la Utendaji		
		2019/20	2020/21	2021/22
Kiwango katika asilimia cha idadi ya watu wanaohudumiwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mugumu	%	53.4	75	80
Kiwango cha idadi ya watu wanaoishi katika eneo lililofikiwa na mtandao wa maji	%	70	70	85
Kiwango cha upotevu wa maji (NRW)	%	26	24	22
Wastani wa muda wa utoaji huduma	Saa	18	20	24
Kiwango cha Wateja wa Dira	%	65	85	100
Kiwango cha Ufanisi wa Ukusanyaji mapato	%	92	95	98

JEDWALI LA NNE

(Limetengenezwa chini ya aya ya 4(k))

MAHITAJI YA FEDHA YALIYOIDHINISHWA (SHILINGI ZA KITANZANIA KATIKA MILIONI)

Maelezo	2019/2020	2020/2021	2021/2022
Uendeshaji na Matengenezo			
Uzalishaji	177.2	180.19	183.25
Usambazaji	136.0	159.70	176.08
Majitaka	26.0	32.10	36.0
Utumishi	182.0	199.20	213.0
Utawala	38.06	42.08	32.50
Matukio na Ufadhili	15.70	16.90	18.90
Gharama za Bodi	41.26	47.60	55.07
Fedha	0.20	0.30	0.30
Jumla ya Uendeshaji na Matengenezo	625.56	692.15	748.95
Uchakavu	48.51	67.51	85.01
Faida ya Uwekezaji	171.14	187.83	189.35
Jumla ya Mahitaji ya Fedha	845.21	947.50	1,023.31
Ondoa: Ufadhili wa Serikali	100.00	120.00	140.00
Ondoa: Mapato Mengineyo	11.01	13.44	15.71
Mahitaji ya Fedha kutoka Mauzo ya Maji	734.21	814.06	867.61

Uzalishaji wa Maji (mita za ujazo)	920,000	920,000	920,000
Kiwango cha upotevu wa maji (%)	26	24	22
Maji yaliyouzwa (m^3)	636,400	675,000	699,200
Wastani wa Bei (Shilingi kwa mita ya Ujazo	1,156	1,167	1,211

Dodoma
14 Novemba, 2019

NZINYANGWA E. MCHANY
Mkurugenzi Mkuu